# For His Glory Ministries

## Mafundisho ya Waafundishaji (T4T) – Kitabu cha Malekezo kuhusu kuwafanya wanafunzi wa Kristo

## I. T4T: Kuzindua Harakati za Kufanya Wanafunzi: Kwa Nini, Vipi na Nini:

**1. Kwa nini:** For His Glory Ministries  ipo ili kusaidia kutimiza matakwa ya mwisho ya Bwana Yesu kwamba tufanye wanafunzi wa mataifa yote. (Mathayo 28:19) Tunawasaidia wachungaji na viongozi wa makanisa kuwaachilia washiriki wao katika huduma kwa kubadilisha mtindo wa kawaida wa kufanya wanafunzi kutoka “kukua kisha nenda” na **“kukua unapoenda”.**

**2. Kwa jinsi gani:** Kiti cha miguu-3 ni sitiari ya mkakati wa pointi 3 tunaotumia kusaidia makanisa ya mtaa kuanzisha harakati za kufanya wanafunzi ili kubadilisha jumuiya zao kwa ajili ya Kristo.

1. Harakati hii huongozwa na kutiwa nguvu na Roho Mtakatifu. ( Matendo 13:2 )
2. Kwamba tuna mamlaka ya Yesu kupitia Jina Lake. (Mathayo 28:18; Matendo 3:6, 16 )
3. Mfano wa T4T wa kufanya wanafunzi wanaofanya wanafunzi. ( Mathayo 28:19-20 )

**3. Nini:** Mtindo huu ni wa kimapinduzi kwa sababu unampa kila mfuasi wa Yesu uwezo wa kushiriki ushuhuda wao wa kile ambacho Yesu Kristo amewafanyia na kufanya wanafunzi. Mfano huu tunauita Mafunzo kwa Wakufunzi (T4T) na unachangia katika kuanzishwa kwa vuguvugu la kiasili la kujiendeleza la kuwafanya watu kuwa wanafunzi hapa na duniani kote.

## Masomo na mazoezi yafuatayo ya T4T yanaweza kutumika wakati wa kuwafunza wengine au katika kuongoza Warsha za T4T.

## 1. KWA NINI tunahitaji kushirikisha Habari njema kwa wengine?

Tumia amri 4 au mwito wa aina 4 kama ifuatavyo:

| **Amri 4** (Matayo 28:19-20) | **Aina 4 za Mwito** |
|---|---|
| 1. Nenda | 1. Mwito utokao <u>Juu</u>: Marko 16:15 |
| 2. Mkawafanye wanafunzi | 2. Mwito utokao <u>Chini</u>: Luka 16:27-28 |
| 3. Wabatize | 3. Mwito utokao <u>Ndani</u>: 1 Wakorinto. 9:16-17 |
| 4. Wafundishe kutii | 4. Mwito utokao <u>Nje</u>: Matendo 16:9 |

## 2. Kwa jinsi gani: Maarifa/ Kutii/ Huduma

## 3. Nini (Kitu gani): Malengo ya mafundisho ni:

1. Kutambulisha T4T mafundisho kwa wafundishaji mkakaati wa kufundisha wanafundi kwa kuzisisha na uwezeshaji wa vkundi vidogo.
2. Kuhamasisha kila mwanfunzi wa kristo na wahudumu kutumia mkakati wa T4T kuwapata na kufundisha mamia, hata maelefu ya waumini wapya.
3. Kuwatia nguvu mpya wafuasi wa Yesu katika jamii yetu tukifanya mabadiliko chanya katika familia, makanisa na sehemu za kazi toka chini kwenda juu.

## 4. Kwa nini: Misingi ya Biblia kuhusu T4T (Training for Trainers)

1. **Mathayo** 28:18-20 –

Mwanfunzi SIYO mwanafunzi mpaka yeye mwenyewe Mke/ Mume anafundisha wanafunzi wanofundisha mengine kuwa wanafunzi.

2. **Matendo ya Roho Mtakatifu kupitia kanisa la mwanzo**
   - Kujumulisha (+) - Matendo 2:41 & 47 (Jumla Kila siku)
   - Kuzidisha (x) - Matendo 4: 32; 6:7

3. **Mkakati wa Mtume Paulo** 2 Timoteo 2:2 –
   - Vizazi vine vya wanafunzi – Paulo > Timoteo > Watu waaminifu > Wengine

## 5. Jinsi gani: Njia nzuri zaidi – Tofauti ya T4T?

1. Fundisha kila muumini ku … Msikilize Roho Mtakatifu.
2. Fundisha kila muumini ku … Shirikisha Imani yake wasioamini.
3. Fundisha kila muumini ku … Fundisha waumini wapya.

## 6. Mwanafunzi wa Kristo ni nani na nini kazi yake:

Mathayo 28:19-20, Yesu anatuambia:

> *"Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*

**Fikiria tafsri ya mwanafunzi katika sehemu tatu**:

> *"Yule anayekubari, akatii, na kumueneza Yesu."*

Mwanafunzi wa Kristo ni Mfuashsi wa Yesu anayewafanya wanafunzi na kuwafundusha jinsi ya kuwafanya wanafunzi wengine.

## II. Historia ya T4T

Bwana alimwambia Ying Kai, “Usiwafanye watu kuwa wanfunzi tu, bali fundisha wengine kuwa wanafunzi” Hatulengi tu watoto wa kiroho tu bali watoto wao wa kiroho. **Kumbukumbu la Torati 4:9:29:29**

## III. Overview of T4T

## IV. Kuwashirikisha wengine: Maswali Manne

1. Natakiwa kusema nini?
2. Ninani nitakayesema naye?
3. Kitu gani kitakachoniwezesha kuwa mwaminifu kufanya hili?
4. Natakiwa nifanye nii iwapo mtu atasema ndiyo kwa Yesu?

1. **Niseme nini?**
    A. Ombea hitaji!

    B. Eleza habari yako.
    Sehemu tatu za habari yako (ushuhuda wako) – Simulia habari yako bila kusikika kama mtu mwenye udini ndani yake.

    1. Maisha yako kabla ya Yesu
    2. Ulikutana je na Yesu
    3. Maisha yako baada ya kukutana na Yesu

    a. Andika habari yako kwa kifupi isizidi dakika harisi na ueleze majeraha na nafsi yako

    b. Fanyia mazoezi ushuhuda wako
    1. Uisome mara mbili kwa sauti
    2. Simulia ushuhuda wako kwa mwenzako
    3. Baada ya mafundisho, wasimulie waumini na rafiki watatu ushuhuda wako na uwaombe wakusaidie malekebisho yanayo hitajika ili kuubiresha.

**2. Nimuelezee nani?**

C. Wowote 3 = Yeyote, Popote, Wakati wowote

1. Jiunganishe: Salam?  Wewe ni nani? Unafanya kazi gani?

2. Ingiza Maongezi ya Mungu: Wewe ni muumini wa gini gani? Wewe ni mu Hindu, Buddhist, Muislam, Mkiristo au dini nyinngine?
3. **Ingiza kupotea kwetu kwetu**: Sema: Karibu Dini zote zinafanana, au siyo? Wote tunajaribu kumpendeza Mungu. Wote tunajitahidi

kwenda mbinguni. Tunajitahidi kushughulikia madhambi yetu? Sisi wote ni wenye dhambi, au siyo?

4. **Ingiza Habari Njema**: Sema: Dini yangu tofauti. Mimi nimekwisha samehewa madhambi yangu najua nitaenda mbinguni. Eleza habari zako ( toa ushuhuda wako na hadithi ya miduara 3)

5. **Elekea kwenye maamuzi**: Warumi 10:9-10 (Muulize; “Umewahi kumpa Yesu Kristo maisha yako?”)

D. **Muulize; “Ungependa kufanya hivo?”**

1. Kama atasema hapana, hakuna shida umepanda mbegu.
2. Wakileta kutokubaliana na wewe, usibishane nao, bali wewe warudishe kwenye upendo wa Yesu na ushuhuda wako.
3. Wakisema ndiyo, washirikishe habari njema (miduara 3) na uwaongoze katika maombi mafupi, kubari ya kwamba ni yenye dhambi na uwahimize kupokea msamaha wa Mungu na Uzima wa milele katika Yesu Kristo.

## 3. Ni kitu gani kitaniwezesha kufanya haya kwa uaminifu?

A. Mariko 6:7-13 - Yesu aliwatuma wanafunzi wake wawili-wawili. (Anzisha kikundi cya T4T)

B. Mariko 6:30-31 – Wanafunzi wake walimletea Yesu habari baada ya kazi. (Hudhuria kwenye kikundi cha T4T)

C. Kuchukulia uwajibikaji wa kila mmoja utatufanya “watumishi na sio wasikilizaji tu.” Yakobo 1:22; Nini maana ya “kutii”? (Sikiliza kutoka rohoni, Kusikiarikiza kwa makini na kifanya kile ambacho Mungu anasema) Mathayo 28: 20

D. Tutakutana “wiki ijayo” au “wiki nyingine” tutaongea kilichotokea. (Taarifa ya kira wiki au ya wiki mbili kwa kikundi cha T4T na kuangalia kile ambacho Mundu ameikifanya kupitia kuwashirikisha wengine Habari njema kwenye mkutano uliopita.)

## 4. Nifanye nini iwapi “Watakubari” kumpa Yesu maisha?

A. Tutawaalika katika mikutano ya kila wiki au wiki mbili ambapo wataanza kufundisha kama Wanafunzi wa Yesu.

B. Tutajifunza masomo rahisi 12 ambayo yatatuwezesha kumuongoza mtu kuanza maisha mapya na Yesu Kristo, na kuwaweka kwenye njia ya maisha marefu katika ukuaji wa mahusiano mazuri na Yesu na Wakristo wengine.
*Haya masomo 12 yameorodheshwa kwenye ukurasa wa 17*

## V. Kuzidisha kuriko Kujumlisha – Mambo ya msingi

**1. Vitu rahisi kuzidisha kiurahisi**

- Vitendea kazi vyote tutakavyo wafundisha wanafunzi kutumia ni rahisi na rahisi kutumia. Yeyote yule anaweza kuvitumia kufundishia wengine. Ukitumia vitendeakazi ambavyo sio rahisi kutumia na kuelewa, hutaweza kuona mwendo wa wanafunzi wa Yesu ukitokea.

**2. Umuhimu wa kuzidisha** – Hatuwezi kumfikia kila mmoja peke yetu

- Tunapaswa kuwafanya wanafunzi wanaofanya wanafunzi wengine
- Tunapaswa kuanzusha vikundi ambavyo vitaanzisha vikundu vingine

**3. Endesha mfumo wa T4T kwa Mazoezi ya Kuzidisha kwa maandiko (mistari) ya Biblia katika kikundi**

## VI. Zaidi kuhusu "Nani", "Nini" na "Kwa jinsi gani" ya kushirikisha wengine Habari Njema

**1. Nani tutakaye mshikirikisha Habari Njema?** Anzia kwa wale ambao una mahusiano nao, yaani maarafiki zako, familiya yako, wale munao husiana, wafanyakazi wenzio, majirani au yeyote yule ambaye mko mahusiano furani hata kama ni kweye mtandao.

- Orodhesha angalau watu 20 ambao unajua ya kwamba hawana mahusiano mazuri na Mungu. Tumia karatasi tupu (moya). Ombea orodha hiyo na umuombe Mungu akupe (akuonyeshe) 5 kati yao ambao utawashirikisha ushuhuda wako na hadithi (habari) ya Mungu katika ijayo.

*Kuna jedwali kwenye ukurasa wa 15 ambalo litakusaidia kufanya hiyo orodha ya watu ambao unawajua na unaweza kuwaombea na kuwashirikisha Habari Njema.


**2. Kwa Jinsi gani tunaweza kushirikisha Habari Njema kwa wengine?**
Pia, unaanza na ushuhuda wako kama daraja la kufikia habari ya Mungu.

- Ni rahisi kuivunja barafu kwa kuanza na maongezi.
  1. Kwa marafiki na Familia anza na kitu kama; "Naweza kuwashuhudia kuhusu kile ambacho kimekuwa kikitokea maishani mwangu?"
  2. Kwa watu ambao umeutana nao kwa mara ya kwanza, vunja barafu kwa kuanza na swali kama; "unafanya kazi gani, au niambie nini maana ya hiyo micholo kwenye mwili wako au nguo yako n.k?"
- Jinsi ya kueleza ushuhuda wako katika au chini ya dakika 3:

1. Eleza maisha yako **Kabla** ya kumfuata.
2. Eleza ni **kwa nini** na **ilikuwaje** ukaamua kumfuata Yesu.
3. Eleza maisha yako **Baada** ya kumfuata Yesu na ni mabadiliko gani ameyafanya katika maisha yako.

- Hakikisha unaomba **jibu** baada ya ushuhuda wako utakao kusaidia kuanzisha habari za Mungu.
- Tumia mfumo wa **Miduara 3** kwa kushirikisha **habari za Mungu (Habari Njema):**

## 3. Nini: Eleza Habari za Mungu, Habarti Njema:
## Mfumo wa Uinjiristi wa Miduala 3




**<u>Haya ni maelezo utakayo yatumia ukichola miduara 3:</u>**
Tunaishi katika ulimwengu huu, ambao umejaa uvunjifu, huhitaji kuchunguza sana kuona kwamba kuna magonjwa, majanga, vita. Familia zilizovunjika kuna maumivu mengi katika Ulimwengu huu, lakini huu sio mpango awali wa Mungu.
Mungu anampango mkamilifu kwa maisha yetu, jinsi tulivyoingia kwenye uvunjifu ni kile Biblia ina ita dhambi. Dhambi ni kuupa kisogo mpango wa Mungu na kufua njia zetu wenyewe, na ndiyo ina tuelekeza kwenye uvunnifu wetu. Uvumilifu badaye inatuelekeza kwa kifo, na kifo kitatutenganisha kutoka kwa Mungu milele. Lakini Mungu hataki tubakie kwenye uvunjifu.

Ameweka njia ya kutokea nje, njia hiyo ni Yesu, Yesu anakuja na kumpa katika uvunjifu wetu na kifo tunachostahili kwa uovu wetu. Yesu anakwenda msalabani na mwili wake unavunjwa kwa mabaya yetu siku tatu baada ya kufa, akafufuliwa toka wafu na kutengeneza njia ya kutokea kwenye uvunjifu. Watu wanajaribu mambo mwengi ili waondokane na uvunjifu. Mambo kama dini, mafanikio, pesa, mahusiano, elimu, ulevi na madawa ya kulevya lakini hakuna jambo lolote kama hili ambao linaweza kutokea kwenye uvunjifu. Njia pekee ya kututoa ni Yesu alikuja jwa ajili yetu na kufufuka toka wafu, ndipo tunaweza kuachana na uvunjifu na kukua katika

mahusiano na Mungu na kufuata mpango kamili kwa maisha yetu tunaweza kutumwa kama Yesu, kusaidia wengine waweze kufuata mpango wa Mungu.
Hapa dunia tuna makundi mawili ya watu, wapo wale wanaofuatia mpango wa Mungu na wale ambao bado wako katika uvunjifu. Tunapaswa tujiulize sisi tuko kundi gani. Sasa wewe unafikiri uko kundi lipi?

1. **Angalia Miduara 3 hapa:** https://www.youtube.com/watch?v=V7mURm-8cOI

## Mfumo wa Uinjilisti wa Miduara 3 kwa Desturi ya Kuongelewa

1. Katika desturi za baadhi ya sehemu za Ulimwengu huu ambapo walio wengi wahawana uwezo wa kusoma au kuandika, utahitaji kutumia mkono wako kueleza miduara 3.

a. Tengezeza mduara ukitumia mikono yako ukisema, “Mungu aliumba Dunia ikiwa imekamirika kwa Binadamu”.

b. Vunja mikono yako ukiachanisha ukisema, “Adam na uasi wetu na dhambi vilileta uvunjifu katika ulimwengu huu”.

c. “Watu hujaribu kujaza uvunjifu kwa kutumia mambo tofauti ya ulimwengu kama vile; Kazi, Anasa, Dini, Uraibu, na mengine mengi lakini hayawezi kuujaza uvunjifu tulio nao.”

d. Fanya mwendo uelekeao chini ukitumia mkono ukisema, “Tusingeweza kwenda kwa Mungu kutokana na dhambi na kwahiyo Mungu aliyejifanya binadamu kupitia Yesu akaja kwetu.”

e. Tengeneza msaraba kwa kutumia mikono ukisema, “Alikufa msarabani kwa ajiri ya dhambi zetu”, fanya mwendo uelekeao juu ukisema; “Alifufuka kutoka kwa wafu akatupa uzima wake wa milele. Kwa hiyo, ukiacha uvunjifu na dhambi na kukiri kwa kinywa chako ya kwamba Yesu ni Bwana na kuamini moyoni mwako kuwa Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, utaokolewa.” Warumi 10:9

f. Unaweza kuwaeleza pia kwamba wanaweza kuelekeza maisha katika kukua katika mahusiano yao na Mungu na Roho wake Mtakatifu ambavyo hukudilisha kuwa kama Mwana wake Yesu kuanzia ndani kueleka nnje.

g. Unaweza kuwajulisha kwamba wakimuamini Yesu; watahisi umwepo wake zaidi na wataishi katika amani bila kujari yanayotokea ulimwenguni.

h. Sawa kama wamemjua Yesu, wanweza kwenda kwa watu ambao bado wanashi katika uvunjifu na kuwashirikisha kile ambacho Yesu amefanya katika maisha yao ili wapate uzima, raha, na amani ambavyo hutolewa na Yesu peke yake.


## VI. Rasilimali:

**Kitabu: Mafundisho ya Wanafunzi ya (na) Ying Kai, au S-T4T Simulizi kinywa la Biblia kwa kutumia T4T**

For More information go to www.forhisglorymin.org www.big.life or www.t4tonline.org

## VII. Mafundisho ya Kuusambaza Ufalme (Kingdom Movements Training (KMT))

Mambo ma 4 ya kuanzisha Usambazaji wa Ufalme wa Kubadilisha Mataifa kwa Kristo




1. Yesu alikuja kuanzisha Ufalme wake na anatumia mambo manne ya Kanisa
    a. Mikutano wa Injili: Kuanzisha rasmi mwamsho (mwendo) wa usambazaji ambao huleta muungano wa Makanisa, **Matendo 2:1**
    b. Kanisa: Mwili (kusanyiko) la waunini, Luka 4:16
    c. Nenda na ukashuhudie: Jukumu kubwa zaidi, **Mathayo 28:18-20**
    **d.** Makundi ya kufanya wanafunzi: Yesu na Mitume 12, **Matendo 2:46**

2. Nenda na Ukashuhudie: Jukumu kubwa zaidi
    a. Tummepewa Mamlaka ya Yesu na kudhihirika tukikubari kwenda, omba na shuhudie
    b. Wengi huja (kwa Yesu) tunapo kwenda
    c. Si kuabudu tu bali, Wanafunzi
    d. Wafundishe wanafunzi kuwafanya wanafunzi wengine
    e. Kikosi kilienda na kushuhudia papo hapo, Mariko:19
    f. Eleza ushuhuda wako, uluza kama wameisha mpa Yesu maisha

g. Eleza habari za Yesu na mfumo wa Habari Njema ya Miduara 3
h. Wafundishe na kuwaandaa katika kuwa na uwezo wa kuwafanya Wanafunzi wengine

3. Makundi ya Wanafunzi: Makundi madogo ya kuwafundusha wanafunzi (Yesu na 12)
    a. Onyesha mfumo wa kundi dogo
    b. Zoezi la kuunda Kundi
    c. Kila mara uliza kila mmoja katika kundi kama wameisha shirikisha Yesu kwa wengine angalau wiki iliyopita na kitu gani kilitokea
    d. Wakumbushe kila mara kuuliza Roho Mtakatifu kila siku kuwatumia mtu aliyeandaliwa njiani mwao
    e. Fanya maombi kwa orodha ya watu 20 hadi 100 au zaidi ya majina ya watu wanaomuhitaji Yesu
    f. Fundisha kundi lako kuhusu malengo ya moyo wa Mungu kwa walio potea
    g. Omba, ukiomba Roho Mtakatifu kukuongoza katika kuandaa jinsi ya kuwafikia Pray, jinsi ya kuwafikia watu 5 kutoka kwenye orodha yako wiki ijayo.

4. Kanisa: kusanyiko la waumini kwa malengo ya kufundisha, kuomba, na kuabudu
    a. Yesu alihudhuria kusanyiko la kwao la kila: **Luka 4:16**
    b. Yesu alianzisha Kanisa ili kuanzisha Ufalme wake Duniani lakini lazima lionekane katika mambo 4 kikamilifu. **Mathayo 16:16-19**
    c. Maono ya kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai ndiye mwamba ambao Kanisa linejengwa juu yake, **Mathayo 16:16**
    **d.** Yesu hutoa Mamlaka ya Ufalme kwa Kanisa, **Mathayo 16:19**

5. Mkutano wa Injili: kuanzisha rasmi mwamko wa kufundisha wanafunzu wanao fundisha wanafunzi wengine.
    a. Kusanyiko la waumini na wasioamini katika jamii kusikia Habari Njema
    b. Huwezesha umoja baina ya Makanisa katika mji
    c. Huunda mazingira ya mafundisho ya wanafunzi kuzidisha na kusambaa katika jamii
    d. Unaweza kusaidia kumtangaza Kristo katika Mji
6. Wanafunzi wanaowafanya wanafunzi wenzine:
    a. Wanafunzi huhitaji kukua wakiwa wanaenda, sio kukua kwanza na kwenda baadae (kabla ya kwenda), tunajifunza vema zaidi kwa kutenda.
    b. Ukienda pole pole utakua pole pole, ukienda haraka utakua haraka
    c. Mafundisho ya makundi madogo ya wanafunzi, huanza yakiwa madogo na baadae hukua na kuwa makubwa
7. Maombi yenye ufanisi ni kitu cha msingi

## VIII. Mafunzo ya T4T ya Kuuzidisha Ufalme: Kuwezeshwa kwa Wachungaji katika Ukuaji wa Matokeo ya Ufalme

**Hatua ya1:** Wachungaji waanao ongoza Wachungaji Viongozi

- Wachungaji huchagua viongozi na kuwaatuma kwenye mafunzo ya T4T.
- Hawa vioongizi wapya hutumwa wawili-wawili katika maeneo jirani yaliyochaguliwa kwa usimamizi wa Mchungaji, ambayo ndiyo maeneo yao ya kufanyia kazi.
- Wanaombea kila familia katila eneo hilo
- Wakifanya maombi wa kutembea katika haya makazi, wanatembelea familia na kufanya urafiki na wakazi wake, wakiomba kukidhi mahitaji yao na kuwashikisha neon na Mungu wakitumia mfumo wa Miduara 3 kila ikiwezekana.
- Wachungaji wasimamizi huwatia moyo viongozi waliowatuma wakiomba Roho Mtakatifu kuwaongoza kwa mtu wa amani katika kila mtaa.
- Viongozi wawili wataendesha mikutano midogo ya mafunzo ya kundi la kuwafanya wanafunzi kila wiki nyumbani kwa "Mtu wa Amani".
- Wataendelea kusimulia kuhusu jinsi walivyo kutana na Yesu, wakiongoza majirani zao kwa Kristo na kuwaalika katika mikutani ya kundi la kuwafanya wanafunzi wa Yesu Kristo kila wiki.

**Hatua ya 2**: Wachungaji waongozao Viongozi wa Viongozi wengine

- Viongozi wanawafundisha washirika wa kundi kwa muundo wa T4T.
- Washirika wa kundi wakifika 10, chini ya uongozi na uamuzi wa Mchungaji atawahadua wawili miongoni mwao na kuwatoa wande kuanzisha na kuliongoza kundi jipya.
- Mchungaji msimamizi atawaongoza katika kuchagua mtaa mwingine jirani ili kurudia zoezi lilelile.
- Ni muhimu kwa Mchungaji msimamizi au kiongizi aliyeteuliwa na Mchungaji kukutana na kila mwanafunzi miongoni mwa wale wanaoandaliwa kuwa viongozi.
- Kiongozi wa kundi-mzazi anapashwa kuwasaidia hao viongoze wapya ili kuhakikisha wanaenda katika mfumo ule ule; Mwendo wa maombi, Kuomba uongozi wa Roho Mtakatifu, na kuongozana na uongozi wa kundi mpya la wanafunzi wa Kristo.

**Hatua ya 3:** Kuongoza Viongozi katika Uzidishwaji wa Uongozi

- Viongozi wenye Uongozi mzuri (wenye afya) wenye kundi la washirika 8 hadi 10, kila iwezekapo wapaswa kutambua wawili miongoni mwao wanao weza kuzidisha viongozi.
- Viongozi pia watawafundisha hawa viongozi wawili wa kizazi kifuatacho katika mfumo wa T4T, kanuni za kuzidisha na mafunzo ya Kuzidisha Uongozi.
- Hawa viongozi wapya wa kuzidisha viongozi wanapaswa kutambulishwa kwa Mchungaji msimamizi au Kiongozi aliyeteuliwa na Mchungaji.

**Hatua ya 4**: Rudia Mchakato wa Kuzidisha Uongozi

- Hawa Viongozi wapya wanao zidishwa watarudia mfumo ule ule wa katika mtaa jirano. Wanafunzi wapya wote watapokea mafundisho ya T4T.

- Kila kiongozi wa kunzi ka wanafunzi atahudhuria mkutano wa mafundisho ya Kuzudushwa kwa Uongozi wa Ufalme wa lika mwezi pamoja na viongozi wengine wa T4T uliopangwa na Mchungaji msimamizi.
- Kila kiongozi mpya atapokea mkono wa usadizi wa kufuatiliaji na viongozi wake kutoka kizazi cha kundi-mzazi.
- Kila mwanafunzi anaye wafanya wanafunzu wengine atahudhuria katika makundi mawili, kundi lao asili ambapao wataweza kukua kiroho na kundi la pili ampapo watafindisha wengine.
- Iwapo makundi ya wanafunzi yatafikia kizazi cha 4 na kundelea, mwamko wa usambazaji wa kuwafanya wanafunzi unaojitosheleza katika wananchi asilia wenyewe utakuwa umeanzishwa!

Hivyo basi, Ufalme wa Mungu utakuwa umeendelea…

## IX. Muhimu kwa Mienendo ya Kuzidisha ya T4T:

1) Viongozi wakuu wa kanisa lazima wapiganie na kuwa mfano wa T4T
   a) Wakumbushe mkutano wako kila mara kumwomba Roho Mtakatifu awaongoze kwa mtu fulani kila siku.
   b) Wafunze waumini wote kwa mamlaka yao katika Jina la Kristo
   c) Wanachama wako hufanya tu kile unachofanya ili kuiga, kutetea na kukuza T4T mara kwa mara
   d) Viongozi wakuu wanapaswa kuongoza kikundi chao cha ufuasi cha T4T cha hadi 12.

2) Mafunzo ya mara kwa mara kwa viongozi wa vikundi vidogo vya ufuasi ni muhimu sana

3) Ni muhimu sana kwamba kila mtu katika kikundi chako cha T4T ajione kama mshiriki wa timu ya Ufalme inayoendeleza kufanya wanafunzi. Kufundisha mara kwa mara ni muhimu.

4) Viongozi wa vikundi wanahitaji kukusanyika kila mwezi katika mkutano mkubwa na kugawanyika katika vikundi vidogo vya uwajibikaji kati ya wanachama 3 hadi 4 wakati wa sehemu ya mkutano

5) Mikutano mikubwa ya kiinjilisti kuwavuta waliopotea inasaidia.

6) Maombi tele ni msingi!

7) Panga saa 2 kila wiki kwa ajili ya uinjilisti (kutembea kwa maombi, mikutano na watu ambao hawajaokoka, au kuhudhuria matukio ya biashara na serikali).

## X. Mkutano wa 3/3 wa kikundi cha T4T wanafunzi wakifanya wengine kuwa wanafunzi:

### Mfumo wa Mikutano ya T4T ya Kila Wiki ya Kufanya Wanafunzi

**Theluthi ya kwanza:** takribani kati ya dakika 20 na 30

1. **Uangalizi wa Mchungaji:** mwachie kila mwanafunzi aeleze nini kinatokea katika maisha yake na familia yake. Watie moyo na waombee.
   ***(uliza unajambo lolote la kumshukuru Mungu au una jambo linalo kusumbiua?).***
2. **Kuabudu:** imba wimbo mmoja au mbili za sifa na kuabudu au soma zaburi moja ***(iwe rahisi iwezekane kurudia).***
3. **Uwajibikaji: waombe wanafunzi wote watoe taarifa juu ya.-**
   a) **Ninani walie mshuhudia (kitu gaji Yesu amewatendea?). je wali amini?**
   b) **Ni nani wamemfundisha?**
   c) **Je wale walio wafundisha na wao wanafunsiha wengine?.**
4. Maono ya wito Mkuu: onyesha vikumbushio vya kibiblia juu ya mwito mkuu. **(Mara kwa mara toa mifano jinsi ya kuwashirikisha wengine)**

**Theluthi ya pili:** takribani kati ya dakika 20 na 30

a. Ugunduzi wa Mafunzo ya Biblia (Discovery Bible Study Method (DBS))
   Kwa mbinu hii, Chagua kifungu cha maandiko toka orodha ya masomo yaliyoandaliwa DBS orodha mwishini maswali ya kumuuliza kila mwanakikundi:
   1. Ulipendezwa na nini katika kile kifungu?
   2. Kitu gani kilikutatiza kwenye kifungu?
   3. **Je, kifungu kinatufundisha nini kuhusu Mungu?**
   4. **Je, kifungu kinatufundisha nini kuhusu watu?**

**Theluthi ya mwisho na ya tatu:** takribani kati ya dakika 20 na 30

5. Mara kwa mara muwe wawili na waulizo wote kwenye kundi kufanya mazoezi ya kumshuhudia mwenzake.

6. **Weka maelengo na Omba:**

   a. **Waongoze wanafunzi kumuomba Mungu awaonyeshe ninani wataenda mshuhudia viki hiloi na ninani watamfundiha.**
   b. **Waombe waandike hayo majina.**
   c. **Wamuombe Roho Mtakatifu aandae moyo ya watu waliomo katika orodha zao za majina.**

Tena: Kila kitu katika mkutani ni muhimu. Ukiufupisha mukutano, utakuwa umefupisha kila kipande, usitoe kipande chochote. Kila mara tumia vipande kamili.

## XI. Kanuni za Mkutano wa Vikundi bya For His Glory vya T4T

### 1. Vidogo na Salama:

**Vikundi viwe vidogo;** vianzishwe kwa watu ambao wanafahamiana, wakutane walipozoea nyumbani, kwenye mgahawa, mahali wanapopenda kama kikundi ni kikubwa, kigwe katika vikundi vidogo vidogo kadhaa watu 3, 4 au 5 watu wote waheshimiwe. Chochote kitakachoshirikishwa kwenye kikao kinabaki hapo hapo.

### 2. Kila mmoja anajifunza kukua binafsi katika kikundi,

Kila mmoja anajifuunza kukua kwa kufanya binafsi haya yafuatayo**:**

1. Kuwalezea wengine habari za Yesu
2. Kujifunza toka kwenye Biblia
3. Kuzungumza na Mungu na kumsikiliza yeye
4. Saidia na tia moyo waumini wengine
5. Kwa ujasiri pombana na mateso na nyakati ngumu

### 3. Mjari kila mmoja kama mwenye Uwezo wa kuzaa Wanafunzi wengine:

Muangalie kila mtu ni muhimu katika kazi ya kufundisha, kabla na baada ya kumpokea Yesu viongozi hawalipwi ujira a hawana elimu maalumu.

### 4. Tii (sikiliza kwa makini) na Fundisha:

Makundi yamejengwa kwa misingi ya kutii, sio kupata maarifa tu. Mfuate Yesu kwa kujifunza na kutii Bbiblia kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Jitoe kwa matendo katika kila mkutano na kupitia mnapokutana tena. Mfanyike wavuvi wa watu kwa kufundisha wengine jinsi ya kujifunza na kutoo vilevile. Hii inafanya mazingira ya kumpenda Yesu kumaanisha kumtii Yesu

### 5. Makundi Mapya kutokana Kulea (Ufuatiliaji) & Kuzidisha:

Lenga kuanzisha vikundi vipya badala ya kufanya vikundi kuwa vikubwa kutana na viongozi wapya wanapo anzisha vikundi vipya. Wafundishe kufanya hivyo kwa wengine wafanye wote wameunganishwa katika kazi ya kumfundisha na kuwajibika inayoendelea. Tumia ule mpango wa MAWL (Model, Assit Watch ans Leave) kuwa saidia wengine kuanzisha vikundi.
Zaa vikundi na zalisha viongozi kwa kuzidisha na sio mgawanyiko wa seli.

### 6. Jadili (changia mawazo) & Gundua:

Focus on the Bible. Mtumaini Roho Mtakatifu kumsaidia kila mmoja agundue maana ya maandiko. Ongoza kwa kuuliza maswali badala ya kuwahubiria jithidi kuona wote wanashiriki. Fanya jitihada na uhakikishe wote wanashiriki.

## XII. Mzunguko wa kufundisha (The Training Cycle – MAWL)

- **Model** - Waonyeshe namana ya kufanya kitu **(wiki 2- 3)**
- **Assist** - Wasaidie kufanya **(Wiki 2-3)**

- **Watch** - Waangalie wakifanya **(miaka 2-3 au zaidi)**
- **Leave** - Waachie kazi.

**MAWL**

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kizazi cha kwanza | M | A | W | L | | | |
| Kizazi cha pili | | M | A | W | L | | |
| Kizazi cha tatu | | | M | A | W | L | |
| Kizazi cha nne | | | | M | A | W | L |

**Pendekezo:** MAWL ni mafundisho ambayo ni kama kunendesha Baiskeli. Unamshikilia mtu anayejifunza kundesha na baadae unamuacha aendeshe peke yake.

## 1. Kuwa mojawapo wa makundi mawili ya T4T:

- Kila mara anzisha kikundi na Mtu wa Amani.

- Utakuwa na msingi wa familia ya kiroho.
    - Watu wazima kuanzia 6-12 katika kundi
    - Usijaribu kuwaleta Wakristo wapya katika kundi lako. Badala yake, wasaidie kuanzisha kundi kutokana na mahusiano yao na watu wengine. Waelekeze jinsi yakufanya hivo kasha uwasaidie kufanya hivo.

- You will always be trying to help others start a new group to be their primary spiritual family.
    - Huu ni mfumo tunaoita wa mfano (kielelezo) na kusaidia. Hivyo basi utajikuta makundi mawili au zaidi ukitoa mifano na kusaidia kuanzisha makundi mapya.

## 2. Anzisha Kikundi na Mtu wa Amani:

1. **Ni kitu gani cha kuchunguza kwa mtu wa amani**

    - Ukalimu (Anakaribisha)
    - Mwenye kiu ya mambo ya kiroho
    - Mwenye maswali ya kutaka kufahamu kitu [siyo kutoa mawazo tu – bali anahitaji kujua juu yako]
    - Yuko radhi kukusanya familia/ kikundi/ jamii ili hujifunza Biblia katika mkao wa kikundi

**2. Kutafuta Watu wa Amani:** Watu wa Amani ni watu wanaopende mambo ya kiroho na wanafungua nyumba zao kwako wako radhi kukaribisha rafiki zao na familia kujifunza Biblia na / au watakuruhusu utumie unakazi yao kwa ajili ya Gikundi.

3. **Tafuta kikundi cha Amamni:** Tafuta vikundi ambavyo tayari vipo na uvifanye kuwa vikundi mfano vikundi vya michezo, vikundi vya wanaume, vikundi vya akinamma, vikundi vya kidini, kuzalisha n.k...

**3. Uwajibikaji/ Vikundi bya kuendeleza uongozi:**

1. Muwe katika vikundi vya jinsia moja. Vunja kikundi kifikapo watu wane [hapa utakuwa na vikundi viwili vya watu wiwili mtarudia mchakato] inafanyika hivi ili kuzidisha kikundi.

2. Kila mmoja achague milango 25 ya maandiko kusikiliza ay kusoma [Jaribu kusoma kitabu chote na kupata muhtasali au sura nzima ya kitabu. Kama ni kitabu kifupi, kisome mara kadhaa].

3. Wakutana kwa wawili na washirikishe ambayo Bwana amewauliza waanze kufanya waache kufanya, rekebisha, au kukua ikiwa na matokeo ya yale walisikiliza.

4. Wananukuu 2 Timotheo 3:16-17 na kushirikisha kile ambacho Bwana amewambia wanapaswa kukifanya, acha kufanya, and share what the Lord has told them they should start doing, stop doing, rekebisha, au kukua kama matokeo ya kile wanacho kisikia.

5. Baadae mkuu **1 Yoh 2:15 – 17** dhambi zozote zinazohusu tama ya mwili, tama ya macho, au kiburi cha maisha kwa wiki iliyopita baadaye washirikishe vile ambavyo Bwana amewawezesha kutimiza mapenzi yake wiki iliyopita.

6. Baadaye wanachukua muda kuombeana mmoja na mwenzake kufatia waliojifunza siku hiyo.

***Kumbuka:*** *kwamba usiri unapaswa kushirikishwa kikamirifu kwa mshirika mpya baada ya kukubaliana.*

## XIII. Mawazo ya Mwisho:

1. Maombi ndio msingi wa haya yote. (Mfano wa Sala ya Bwana)
2. Maombi yetu ya kibinafsi huishi, wakati katika Neno na kwa Roho ndio ufunguo!
3. Kutembea kwa maombi kunaweza kusaidia kukuza kikundi chako na kubadilisha ujirani.
4. (Somo la John Devries Kaya 80 zisizo na maandalizi ya maombi dhidi ya 80 pamoja na maandalizi ya maombi ambapo 67 walikuwa wazi kuombewa na 40 walikuwa tayari kutembelewa na mshiriki wa kanisa.)
5. Maneno ya mwisho ya Yesu ni muhimu kufuata na pengine ni wapi tutapata utimilifu mkubwa zaidi maishani. (Matendo 1:1-9)
6. Uanafunzi na kufanya wanafunzi ni mtindo wa maisha
7. Tunataka kufanyia kazi Vikundi vinavyozalisha. Ukianzisha Kikundi ambacho hakizai tena, usijali! Jaribu tu tena. Bado ni nuru gizani!
8. “Kila Mkristo ni mmishenari; kila asiye Mkristo ni uwanja wa misheni.” W. Pratney

## Masomo ya kwanza kumi na mawili ya T4T

| | | |
|---|---|---|
| 1. Yesu Akimponya aliyepooza | Luka 5: 17-26 | Nguvu za Zinapomya Kimwili na Kiroho |
| 2. Mabikla kumi | Mathayo 25: 1-13 | Kuhubiri injili |
| 3. Mwana Mpotevu | Luka 15: 1-32<br>(Yohana 1:12, Yohana 10: 27-30) | Hakikisho la Wokovu |
| 4. Kiongozi kutoka Ethiopia | Matendo 8: 25-40 | Kuhubiri injili, Utiifu, **Ubatizo** |
| 5. Yesu akimuita Mwanafunzi wa kwanza | Luka 5: 1-11 | Utiifu, Kuhubiri injili |
| 6. Watimishi watumwa kazini | Luke 10: 1-11, 16-20 | Kuhubiri injili, Hakikisho |
| 7. Mlo wa jioni wa mwisho | Mathayo 26: 26-35 | **Meza ya Bwana** |
| 8. Pentecoste | Matendo 2: 1-13 | Roho Mtakatifu, Mungu abariki Kanisa |
| 9. Yesu na Nikodemu | Yohana 3: 1-21 | Kuhubiri injili |
| 10. Sauli Abadirika kuwa Paulo | Matendo 9:1-19 | Uwezo wa Mungu, Utiifu |
| 11. Wanafunzi wataka kuwa wa kwanza<br>Yesu awaosha miguu wanafunzi | Marko 9: 33-37<br>Yohana 13: 5-13 | Majivuno (Kiburi)<br>Utumishi |
| 12. Kujaribiwa kwa Yesu | Luka 4: 1-13 | Kuyashinda Majaribu kwa Neno la Mungu |

## ORODHA (LIST) YA UTAKAO WAOMBE

Orodhesha watu 20 unaowajua ambao sio Wakristo. Jaribu hata 100. Unaweza hata kutumia nyuma ya karatasi.

| | |
|---|---|
| 1. ______ | 26. ______ |
| 2. ______ | 27. ______ |
| 3. ______ | 28. ______ |
| 4. ______ | 29. ______ |
| 5. ______ | 30. ______ |
| 6. ______ | 31. ______ |
| 7. ______ | 32. ______ |
| 8. ______ | 33. ______ |
| 9. ______ | 34. ______ |
| 10. ______ | 35. ______ |
| 11. ______ | 36. ______ |
| 12. ______ | 37. ______ |
| 13. ______ | 38. ______ |
| 14. ______ | 39. ______ |
| 15. ______ | 40. ______ |
| 16. ______ | 41. ______ |
| 17. ______ | 42. ______ |
| 18. ______ | 43. ______ |
| 19. ______ | 44. ______ |
| 20. ______ | 45. ______ |
| 21. ______ | 46. ______ |
| 22. ______ | 47. ______ |
| 23. ______ | 48. ______ |
| 24. ______ | 49. ______ |
| 25. ______ | 50. ______ |